JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA YA MWAKA KWA MWAKA 2016/2017 SEKTA YA UVUVI MKOA WA LINDI

KUANZIA JULAI 2016 – JUNE, 2017

Imetayarishwa na:
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi
S.L.P. 1054
LINDI

Simu: 023-220-2098
Fax: 023-220-2502
Barua pepe:ras.lindi@pmoralg.go.tz, 2017.

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI 3
2.0 UTEKELEZAJI WA SERA, SHERIA NA MIKAKATI YA UVUVI 4
2.1 Uzalishaji na Ufugaji wa Samaki Kwenye Mabwawa 4
2.2 Usajili wa Vyombo Vya Uvuvi 5
2.2.1 Usajili wa leseni za Wavuvi 5
2.3 Takwimu za Uvunaji na Uuzaji samaki 6
2.4 Ukusanyaji wa Mapato 7
2.5 Udhibiti wa Uvuvi Haramu 8
2.6 Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi 9
2.6.1 Ukaguzi Katika Viwanda, Masoko na Maghala ya Samaki 9
2.6.2 Usimamizi wa Masoko na Mialo ya Samaki 10
3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI 11
4.0 KUELIMISHA JAMII JUU YA ATHARI ZA UVUVI HARAMU NA 13
UKIMWI 13
5.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA 13
6.0 CHANGAMOTO ZILIZOPO 14
7.0 MAPENDEKEZO 16

1.0 UTANGULIZI

Mkoa wa Lindi una mwambao wa bahari usiopungua urefu wa km 285 kutoka Kijiji cha Sudi (Kusini mwa Wilaya ya Lindi) mpaka Kijiji cha Marendego (Kaskazini mwa Wilaya ya Kilwa). Ukanda huu wa Bahari una fukwe nyingi zinazofaa kwa ufugaji wa viumbe vya majini kama vile samaki, Kaa, Chaza na kilimo cha Mwani. Vilevile Mkoa una hekta 10,275 zinazofaaa kwa umwagiliaji na eneo hilo linafaa kwa ufugaji samaki wa maji baridi. Wananchi wengi hutegemea shughuli za uvuvi kuwaingizia kipato, uvuvi ambao hutumia zana, vyombo na teknolojia duni, ambayo huwalazimisha kuvua karibu na pwani (Inshore Water). Vyombo hivyo ni mashua, madau, ngalawa na mitumbwi (dugout cones) vinavyoendeshwa ama kwa kutumia matanga (upepo) au makasia. Mkoa una vyombo vya Uvuvi **2,404** na wavuvi wenye leseni hadi kufikia mwezi juni 2017 mkoa ulikuwa na wavuvi **7,923**. Zana nyingine za Uvuvi zinazotumika ni pamoja na madema, wando, zurumati, mishipi ya mkononi, nyavu ndogo za jarife na nyavu za kilindini za kuzungusha makundi ya samaki (Purse-seines), vimia na nyavu za dagaa.

Uvuvi mdogomdogo hutoa asilimia 98 ya mavuno ya mazao ya baharini ya Mkoa, aidha uvuvi wa bahari hutoa asilimia 94 kwa samaki wote wanaovuliwa Mkoani. Inakadiliwa kwamba asilimia 50 – 70 ya wakazi wa mwambao na 30 – 45 ya wakazi wa mbali na bahari wanategemea protini itokanayo na samaki. Ulaji wa samaki kwa mwaka kwa mtu unakadiriwa kati ya kilo 8 hadi 12.

Ufugaji Samaki huchangia kati ya asilimia 2 - 5 ya uvuvi wote unaofanyika kwa mwaka, Uvuvi huu hufanyika katika mito, maziwa madogo, mabwawa ya asili na mabwawa ya kuchimba. Aina ya samaki wanaovuliwa na wanaofugwa ni Tilapia na Kambale, Mkoa una jumla ya mabwawa ya kufugia samaki **261**.

2.0 UTEKELEZAJI WA SERA, SHERIA NA MIKAKATI YA UVUVI

Mkoa wa Lindi ni mojawapo ya mikoa inayotekeleza sera ya uvuvi ya mwaka 2015, sheria ya uvuvi Na.22 ya mwaka 2003, Kanuni za uvuvi za mwaka 2009 pamoja na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali kwa lengo la kuhakikisha shughuli za uvuvi zinazofanywa na wananchi zinazingatia taratibu zilizowekwa kwa lengo la kuwepo na matumizi endelevu katika rasilimali za uvuvi ili jamii iweze kunufaika kwa kizazi kilichopo sasa na baadaye. Katika kuzingatia hili, Mkoa kupitia halmashauri zake za Kilwa, Lindi na Manispaa ya Lindi umekuwa ukihimiza wavuvi na wadau wote juu ya kufuata taratibu hizo zilizowekwa na Serikali kabla na wakati wa kufanya shughuli zao, ikiwemo kuhakikisha wavuvi wote wanakuwa na leseni za uvuvi, vyombo vya uvuvi vyote vinasajiliwa, wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi wanakuwa na vibali vya kusafirisha mazao yao ya uvuvi pamoja na kutumia zana za uvuvi zinazokubalika kwa mujibu wa sheria. Suala la ufugaji wa samaki pia limepewa kipaumbele kwa lengo la kupunguza shinikizo la kutegemea samaki watokao kutoka Baharini pekee.

2.1 Uzalishaji na Ufugaji wa Samaki Kwenye Mabwawa

Jedwali Na. 1: Takwimu za mabwawa ya Ufugaji wa samaki Mkoa wa Lindi

Na	Wilaya	Malengo	Mabwawa Yaliyopo (a)	Mabwawa Mapya (b)	Jumla (a + b)	Watu Waliopewa Elimu	Samaki Waliopandikizwa
1	Manispaa Lindi	250	176	3	179	144	66,450
2	H/W Lindi	62	29	7	36	30	-
3	H/W Kilwa	50	4	0	4	30	11,600
4	H/W Nachingwea	20	17	0	17	134	-
5	H/W Ruangwa	5	1	0	1	15	-

6	H/W Liwale	25	20	4	24	200	-
	JUMLA	**412**	**247**	**14**	**261**	**553**	**78,050**

2.2 Usajili wa Vyombo Vya Uvuvi

Jedwali Na. 2: Takwimu za Vyombo vya kuvua samaki Mkoa wa Lindi

NA	**H/WILAYA**	**Jumla ya vyombo vyote vya Kuvua samaki**	**Vyombo vilivyosajiliwa**		**Vyombo ambavyo havijasajiliwa**
			Vyombo vya Kasia	**Vyombo vya Injini**	
1	Manispaa Lindi	304	191	25	93
2	H/W Lindi	237	159	8	71
3	H/W Kilwa	1,863	1,079	229	555
4	H/W Nachingwea	-	-	-	-
5	H/W Ruangwa	-	-	-	-
6	H/W Liwale	-	-	-	-
	JUMLA	**2,404**	**1,429**	**262**	**719**

2.2.1. **USAJILI WA LESENI ZA WAVUVI**

NA	**H/WILAYA**	**Jumla ya Wavuvi wote kwenye H/W**	**Wavuvi wenye Leseni**	**Wavuvi wasio na Leseni**
			Hadi kufikia Apr – June 2017	
1	Manispaa Lindi	871	790	81
2	H/W Lindi	641	335	306
3	H/W Kilwa	7,123	6,798	325
4	H/W Nachingwea	-	-	-
5	H/W Ruangwa	-	-	-

6	H/W Liwale	-	-	-
	JUMLA	**8,635**	**7,923**	**712**

2.3 Takwimu za Uvunaji na Uuzaji wa Samaki

Jedwali namba 5: Takwimu za uvunaji na uuzaji wa samaki Mkoa wa Lindi

Jedwali 5.1SAMAKI WA BAHARINI

WILAYA/ Mwaka	**Samaki Waliovuliwa kwenye Bahari (Kg).**		**Samaki Waliouzwa (Kg).**		**Fedha Zilizopatikana (Tsh)**	
	2015/2016	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**
Manispaa Lindi	284,757	144,501.9	284,757	144,501.9	854,271,000	650,258,550
H/W Lindi	8,554	24,470	8,554	24,470	38,493,000	97,190,500
H/W Kilwa	899,781.75	2,171,973	856,935	2,068,546	3,717,032,310	8,274,184,000
JUMLA	**1,193,092.75**	**2,340,944.9**	**1,193,092.75**	**2,237,517.9**	**4,609,796,310**	**9,021,633,050**

Jedwali 5.2 SAMAKI WA KUFUGA KWENYE MABWAWA

WILAYA/ Mwaka	**Samaki Waliovuliwa kwenye Mabwawa (Kg).**		**Samaki Waliouzwa (Kg).**		**Fedha Zilizopatikana (Tsh)**	
	2015/2016	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**
Manispaa Lindi	**2,843**	**5,553**	**2,843**	**5,553**	**17,058,000**	**2,776,500**
H/W Lindi	**2,039**	**7,809**	**2,039**	**7,809**	**12,234,500**	**28,076,800**
H/W Kilwa	**75**	**-**	**75**	**-**	**450,000**	**-**
H/W Nachingwea	**4,846**	**526**	**4,846**	**526**	**38,768,000**	**4,734,000**

H/W Ruangwa	**0**	**0**	**0**		**0**	**-**
H/W Liwale	**0**	**200**	**0**	**200**	**0**	**1,200,000**
JUMLA	**9,803**	**14,088**	**9,803**	**14,088**	**68,510,500**	**36,787,300**

Halmashauri ya wilaya ya Kilwa haikutoa takwimu za mavuno vilevile Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa haikuleta taarifa kutokana hakuna mtumishi wala mhusika wa kuhudumia sekta hii ya uvuvi.

Jedwali 5.3 KILIMO CHA MWANI

WILAYA/ Mwaka	**Kiasi cha mwani kilichovunwa.**		**Kiasi cha mwani killichouzwa (Kg).**		**Fedha Zilizopatikana (Tsh)**	
	2015/2016	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**	**2015/2016**	**2016/2017**
Manispaa Lindi	2,000	5,379.5	2,000	5,379.5	1,400,000	3,089,750
H/W Lindi	79,644	94,000	79,644	94,000	55,750,800	2,108,750
H/W Kilwa	250,000	820,000	150,000	820,000	105,000,000	20,500,000
JUMLA	**331,644**	**919,379.5**	**331,644**	**919,379.5**	**162,150,800**	**25,698,500**

N.B: Chanzo cha taarifa ni wafanya biashara wa samaki, wafugaji wa samaki kwenye mabwawa na wavuvi.

2.4 Ukusanyaji wa Mapato

Jedwali Na 3: Ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha 2016/2017

MAKUSANYO YA MAPATO KWA MWAKA 2016/2017 (TSHS)								
Na	**WILAYA**	**Malengo kwa mwaka (a)**	**Ada za Leseni/ Vibali (b)**	**Tozo za Faini (c)**	**Maduhuli (d)**	**Makusanyo Mengine (e)**	**Jumla (f=b+c+d+e)**	**% (f/a)**
1	Manispaa Lindi	27,700,000	10,060,000	0	14,490,250	3,300,000	27,850,250	103

2	H/W Lindi	38,338,000	10,046,882	525,000	7,119,150	3,400,950	21,091,982	55
3	H/W Kilwa	114,850,000	102,987,700	0	0	0	102,987,700	89.7
4	H/W Nachingwea	3,000,000	150,000	0	1,875,000	0	2,025,000	67.5
5	H/W Ruangwa	-	-	-	-	-	-	-
6	H/W Liwale	-	-	-	-	-	-	-
JUMLA KUU		**189,888,000**	**123,244,582**	**525,000**	**23,484,400**	**6,700,950**	**153,954,932**	**81**

2.5 Udhibiti wa Uvuvi Haramu

Jedwali Na. 4: Takwimu ya Zana Haramu za Uvuvi zilizokamatwa

WILAYA	**Idadi ya Doria**	**IDADI YA ZANA HARAMU ZILIZOKAMATWA**							**Aina nyingine ya zana zilizokamatwa**	**Watuhumiwa**
		Kokoro	**Vyombo**	**Vilipuzi**	**Mbolea (Kg)**	**Mashine za boti**	**Mitungi ya gesi**	**Mideke**	**Idadi ya samaki (kg)**	
Manispaa Lindi	23	14	0	0	0	0	0	8	135	6	6
H/W Lindi	6	1	0	3	0	0	0	3	185	6	121
H/W Kilwa	20	36	4	6	204	8	18	45	200	3	16
JUMLA	**49**	**51**	**4**	**9**	**204**	**8**	**18**	**56**	**520**	**15**	**143**

2.6 Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi

NA	H/WILAYA	Masoko/Mialo iliokaguliwa	Masoko/Mialo isiokaguliwa	Masoko /Mialo inayofanya kazi	Masoko /Mialo isiyofanya kazi
01.	Manispaa Lindi	14	0	14	0
02.	H/W Lindi	2	0	2	0
03.	H/W Kilwa	4	2	6	0
	JUMLA	20	2	22	0

2.6.1 Ukaguzi Katika Viwanda, Masoko na Maghala ya Samaki

Jedwali Na. 5: Takwimu za Viwanda vya Kuchakata Samaki

WILAYA	JINA LA KIWANDA	UZALISHAJI KWA SIKU (TANI)	UWEZO WA KIWANDA (TANI/SIKU)	AINA YA SAMAKI	MAHALI KILIPO
Manispaa Lindi	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
H/W Lindi	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
H/W Kilwa	Alphakrust	1-3	3-6	Pweza, Samaki, Kamba koche na kamba miti.	Kivinje
H/W Nachingwea	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
H/W Ruangwa	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
H/W Liwale	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna

2.6.2 Usimamizi wa Masoko na Mialo ya Samaki

Jedwali Na. 6: Takwimu za bei ya samaki Mkoa wa Lindi

NA	WILAYA	Idadi Ya Masoko / Mialo	WASTANI WA BEI YA SAMAKI KWA KILO (Tshs/Kg)							
			Samaki wa Baharini		Samaki wa kufugwa		Dagaa		Samaki wengine	
			Bichi	Kavu	Bichi	Kavu	Bichi	Kavu	Bichi	Kavu
1	Manispaa Lindi	14	5,000	6,000	7,500	7,000	3,000	3,500	-	-
2	H/W Lindi	2	3,500	4,500	4,000	5,000	4,000	7,000	4,000	5,500
3	H/W Kilwa	6	4,000	4,500	4,000	4,000	2,500	3,600	4,000	4,500
4	H/W Nachingwea	1	9,000	10,000	9,000	10,000	-	7,000	9,000	10,000
5	H/W Ruangwa	-	-	-	-	-	-	-	-	-
6	H/W Liwale	-	-	-	-	-	-	-	-	-
	WASTANI		**5,500**	**6,000**	**6,000**	**6,500**	**3,000**	**5,000**	**5,500**	**6,000**

Halmashauri za wilaya ya Ruangwa na Liwale hazikuleta takwimu hizi kutokana na kukosa maafisa uvuvi katika maeneo yao.

Jedwali Na.6.1 Uundaji wa vikundi

Na	Wilaya	Idadi ya vikundi vya uvuvi	Idadi ya vikundi vya ufugaji samaki Maji chumvi	Idadi ya Vikundi vya ufugaji wa samaki maji baridi	Idadi ya vikundi vya ukulima wa mwani	Idadi ya BMU	Wastani wa wanachama kwa kikundi
1	Manispaa Lindi	14	12	4	3	13	10
2	H/W Lindi	8	5	2	0	9	15
3	H/W Kilwa	**8**	**0**	**2**	**6**	**16**	**15**
4	H/W Nachingwea	**-**	**-**	**-**	**-**	**-**	**-**
5	H/W Ruangwa	**0**	**0**	**1**	**0**	**0**	**15**
6	H/W Liwale	**-**	**-**	**14**	**-**	**-**	**15**
	Jumla	**30**	**17**	**23**	**9**	**38**	

3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI

Jedwali Na. 7: Takwimu za miradi mbalimbali Mkoa wa Lindi

NA.	WILAYA	AINA YA MRADI	UFADHILI	UTEKELEZAJI

1	Manispaa Lindi	Miradi ya Uvuvi	-MACEMP -WAMA -TASAF Wanakikundi/Jamii	Miradi mingi kwa sasa inatekelezwa na wananchi baada ya wafadhili kukamilisha sehemu yao.
2	H/W Lindi	1. SWIOFISH	Benki ya Dunia	-Sensa ya Uvuvi ilifanyika Machi 2016. -Wavuvi wameandikishwa kwenye daftari kwa ajili ya kufanya uchaguzi wa viongozi na wajumbe wa BMUs. BMUs zipatazo 7 zilihuishwa na moja iliundwa kati ya vijiji vya uvuvi. -Mafunzo yametolewa kwa viongozi wa wa vikundi 3 vya BMU kuhusu utaratibu na uendeshaji wa BMUs -Ugawaji wa vitendea kazi (shajala) kwa ajili ya matumizi ya BMUs.
		2. Ujenzi wa mialo ya shuka na mchinga II.	Halmashauri ya Wilaya.	-Ujenzi upo kwenye hatua ya msingi wa jengo la mwalo wa shuka. -Ujenzi wa jengo la mwalo wa mchinga upo kwenye hatua ya kupauwa kwa bati mpya kabla ya ukarabati wa jumla kuendelea.
03.	H/W Kilwa	WWF Fisheries Co-Management Project	WWF	Uanzishwaji wa BMUs

04.	H/W Nachingwea	Hakuna	Hakuna	Hakuna
05.	H/W Ruangwa	Hakuna	Hakuna	Hakuna
06.	H/W Liwale	Hakuna	Hakuna	Hakuna

4.0 KUELIMISHA JAMII JUU YA ATHARI ZA UVUVI HARAMU NA UKIMWI

Halmashauri zote zilizopo kwenye ukanda wa mwambao mwa Bahari ya Hindi kupitia mikutano yao ya jamii ya wavuvi ilitoa taarifa za utoaji wa elimu juu ya athari za matumizi ya uvuvi haramu wa kutumia milipuko ambayo huharibu mazingira ya Bahari pamoja na kuhatarifa afya za walaji wa samaki. Jumla ya wafugaji samaki **553** na wavuvi **7,923** wenye Leseni za Uvuvi walipatiwa elimu ya uvuvi haramu na athari za maambukizi ya Ukimwi na Elimu ya ugonjwa wa UKIMWI kwa ujumla.

5.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

Pamoja na changamoto zilizopo kwenye sekta hii ya Uvuvi Mkoa wa Lindi umeweza kufanikiwa kwenye mambo yafuatayo:-

i) Kuwepo kwa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato kwa kupitia kwenye Halmashauri kwani kulikuwa na jumla ya lengo la Tsh. **189,888,000/=** ambapo makusanyo yalikuwa **153,954,932/=** sawa na asilimia **81%** ya lengo lililowekwa.

ii) Ongezeko la shughuli za uvuvi kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wavuvi kutoka wavuvi **8,052** waliokuwepo mwaka 2015/2016 hadi kufikia wavuvi **8,635** kwa mwaka huu wa 2016/2017 sawa na asilimia

7.2%, sambamba na ongezeko la idadi ya vyombo vya uvuvi kutoka vyombo **2,367** vilivyokuwepo mwaka 2015/2016 hadi kufikia vyombo **2,404** mwaka 2015/2016 sawa na asilimia **1.6%.**

iii) Idadi ya mavuno kupitia uvuvi wa samaki baharini yameongezeka kutoka kilo **1,193,092.75** mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo **2,340,944.9** kwa mwaka huu 2016/2017.

iv) Idadi ya mavuno kupitia ufugaji wa samaki imeongezeka kutoka kilo 9,803 mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo 14,088 kwa mwaka huu 2016/2017 sawa na asilimia 43.7%.

v) Idadi ya mavuno kupitia kilimo cha mwani imeongezeka kutoka kilo 331,644 mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo 919,379.5 kwa mwaka huu 2016/2017.

vi) Jumla ya doria **49** zilifanyika kupitia Halmashauri za Kilwa, Lindi na Manispaa ya Lindi ambazo zilifanikisha kukamata nyavu za kokoro **51**, vyombo vya uvuvi **4,** vilipuzi **9**, mbolea aina ya urea kilo **204**, mashine za boti **8,** mitungi ya gesi **18,** mideke **56,** samaki kilo **520** pamoja na kukamatwa kwa watuhumiwa **143** ambao walifikishwa kwenye vyombo vya sheria.

6.0 CHANGAMOTO ZILIZOPO

Pamoja na mafanikio mengi yalioonekana kwa kipindi hiki lakini pia Mkoa unakabiliwa na changamoto zifuatazo kupitia Sekta ya uvuvi:-

- Kutokuwepo kwa Boti imara za kufanyia doria pamoja na kikosi maalum cha doria Mkoani, mara nyingi kinachotumika hutokea Dar es Salaam au Mtwara na hufanya kazi kwa muda kisha huondoka.

- Doria inahitaji rasilimali fedha nyingi za kugharamia mafuta ya gari na kukodi boti, Polisi na Maafisa uvuvi, baadhi ya Halmashauri hazitengi fedha

kwa ajili ya ulinzi wa Rasilimali hii ya Bahari hivyo kupelekea suala la Uvuvi haramu kuwa sugu kwenye maeneo yao.

- Upotoshaji wa makusudi uliokuwepo kwa muda mrefu kuwa uanzishaji wa vikundi vya Ulinzi Shirikishi (BMU) ulimaanisha bahari inauzwa (hasa katika Wilaya ya Kilwa).hivyo kusababisha vijiji vingi kuchelewa kuanzisha ama kutokuwa na BMU katika maeneo yao na hatimaye maeneo mengi kuwa maficho ya wavuvi haramu wa baruti na hukimbilia huko baada ya kufanya uhalifu katika maeneo mengine ya Mkoa.

- Kuendelea kutumia zana duni za uvuvi kunasababisha pato la mvuvi kuendelea kuwa dogo,

- Matumizi yasiyo sahihi ya malighafi za kutengeneza zana za uvuvi, mfano mshipi wa plastiki (monofilament) kutumika kutengeneza nyavu ambazo ni hatari kwa uhifadhi wa Mazingira ya Bahari.

- Ukosefu wa maduka ya vifaa bora vya uvuvi.
- Ukosefu wa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) vya wavuvi
- Huduma za ugani na ushauri kuwa finyu kutokana na uhaba wa watumishi na vitendea kazi (Halmashauri za Ruangwa na Liwale hazina kabisa watumishi ingawa kuna mahitaji makubwa kwa wananchi wa maeneo hayo)

- Mabwawa mengi ya kufugia samaki kuwa mbali na makazi hivyo kuwa vigumu kwa mmiliki kuyatunza ipasavyo na kumarisha ulinzi.

- Gharama kubwa za upatikanaji na uandaaji wa chakula cha ziada cha samaki, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iendelee kutoa chakula cha ruzuku kwa wafugaji.

- Ukataji wa mikoko na uharibifu wa mazingira inapelekea vyanzo vya mazalia ya samaki kuendelea kuharibika.

- Fikra potofu za wafugaji kuwa kila kitu kinafanywa na Serikali ama Tasisi (fikra tegemezi).

- Tatizo la ukame na mabadiliko ya hali ya Hewa kupelekea shughuli za ufugaji wa samaki kurudi nyuma (Wilaya za Nachingwea, Liwale na Ruangwa).

- Kutopatikana kwa urahisi mbegu bora/vifaranga vya samaki, Wizara iendelee kuboresha kituo cha uzalishaji wa mbegu bora cha Mtama na kuanzisha kituo kama hicho kwa wafugaji wa samaki aina ya Mwatiko kwa maji chumvi (Mariculture) kwani mahitaji kwa sasa yamekuwa ni makubwa (Wilaya za Lindi na Kilwa).

- Utoaji wa pembejeo kwa ajili ya kilimo cha Mwani kunakofanywa na wanunuzi wa Mwani kwa wakulima kuna haribu zana ya soko huria na kumdhalilisha mkulima kwa kumjengea tabia tegemezi.

- Tatizo la wanunuzi/Makampuni yanayonunua mazao ya uvuvi hasa zao la Mwani kuficha takwimu halisi za manunuzi kwa mamlaka husika kunapelekea kutokwa na usahihi wa takwimu na maendeleo kwenye zao hilo.

7.0 MAPENDEKEZO

Ili kufikia malengo yaliowekwa katika kuendeleza sekta kwa ujumla na kutokana na hali halisi ya sekta ya Uvuvi katika Mkoa wetu ukilinganisha na changamoto zilizopo kwenye Halmashauri zetu, Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) hazina budi kusimamia na kuendeleza rasilimali za Uvuvi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i) MSM zitambue kuwa jukumu la usimamizi wa rasilimali za uvuvi ni la Halmashauri husika kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa kwake, hivyo taasisi, chombo, kikundi au mtu yeyote Yule anayejishughulisha na shughuli za utunzaji, Usimamizi na uendelezaji rasilimali hizo anasaidia tu, Halmashauri hazina budi kutimiza wajibu wake huu muhimu. Kutokana na ukweli huu, kila Halmashauri ijipange na kutengeneza mfumo wa kushirikiana na kushirikisha taasisi zote na vikundi vyote vilivyopo.

ii) Kila Wilaya iandae na isimamie kupitia kamati zake za Ulinzi na Usalama mkakati wa kuondoa kabisa uvuvi haramu katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuwatambua kwa majina wananchi wote wanaojishughulisha na Uvuvi haramu, sambamba na kuwaita na kuwataka kuacha mara moja uvunjaji huo wa sheria za nchi.

iii) Ili kuwa na mwelekeo sahihi na kurahisisha ufuatiliaji, kila Halmashauri iandae mpango mkakati wa sekta ya uvuvi na kuainisha vipaumbele na maeneo ya kimkakati ambayo Halmashauri inajipanga kusimamia.

iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziweke makadirio sahihi ya mapato yatokanayo na Uvuvi na itenge fedha za kutosha na kuelekeza bajeti ya maendeleo kwenye vipaumbele vya pamoja na vinavyoleta matokeo. Katika kutekeleza azma hii, kila Halmashauri itenge walau 15% ya mapato yatokanayo na uvuvi ili yaweze kutumika kuendeleza sekta ya uvuvi.

v) Ili kupunguza malalamiko yanayotolewa na maafisa uvuvi kuhusu sekta ya uvuvi kutoendelezwa, viongozi na watendaji wakuu wote kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa watumie nafasi zao kuwaelimisha na kuwawezesha wataalamu wa sekta ya uvuvi kwenye maeneo yao kutambua kuwa DHAMANA ya sekta ya Uvuvi kwenye eneo la utawala la wilaya iko mikononi mwao.

vi) Ili kujenga uelewa wa kutosha na kuwa na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za uvuvi, kila Halmashauri iandae muhtasari wa sheria ya uvuvi

kwa kuainisha maeneo muhimu ya kuwajengea uwezo viongozi na watendaji wakuu wa wilaya na Halmashauri pamoja na kuwafahamisha wana siasa umuhimu wa sekta ya uvuvi kwa maendeleo ya nchi yetu na kuwataka wote kuelewa kuwa masuala ya KISHERIA na KITAALAMU hayapaswi kuingiliwa isipokuwa kwa kubadilisha sheria.

vii) Kila Halmashauri itunge na kusimamia sheria ndogo za kutunza na kusimamia rasilimali za uvuvi na zitakazohakikisha kuwa wataalamu na watendaji wote wanakuwa na UTAIFA, UZALENDO, UWAJIBIKAJI na wanazingatia MAADILI ikiwa ni pamoja na kulinda na kuheshimu TAALUMA.

viii) Halmashauri isimamie, kuviwezesha na kuvifuatilia vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuhakikisha juhudi za pamoja zinafanyika ili kupata rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya uvuvi, hili liende sambamba na kuangalia uwezekano wa:-

a) Kurudisha asilimia Fulani (15%) kutoka kwenye makusanyo kwa sekta husika ili ziweze kusaidia kuendeleza sekta.

b) Kuona uwezekano wa kuvipatia vikundi vya Usimamizi wa rasilimali za uvuvi uwakala wa kukusanya mapato ili viweze kuwa endelevu.

c) Kuandika maandiko ya kuomba fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

d) Kubuni mbinu nyingine zozote zinazoweza kuongeza rasilimali fedha kwa sekta ya Uvuvi.

ix) Ili kurahisisha usimamizi wa pamoja wa shughuli za utekelazaji wa miradi, Halmashauri zitambue wadau wengine wa sekta ya uvuvi na kuwashirikisha kikamilifu katika kufuatilia vipaumbele/malengo ikiwa ni pamoja na kuainisha kwa kupitia bajeti mchango wa wadau hao wa sekta, na kila Halmashauri iweke utaratibu maalum wa kutunza na kuendeleza miradi, miundombinu na zana za uvuvi zilizowekwa/kununuliwa ili ziwe endelevu na kuwezesha sekta kukua.

x) Kutokana na mahitaji makubwa ya kupata utaalamu wa kufuga samaki katika Halmashauri za wilaya ya Ruangwa na Liwale kuongezeka ni

vema sasa Halmashauri hizo zikafikiria kuajiri watumishi wa sekta ya Uvuvi watakaosaidia kutoa utaalam katika Halmashauri zao.

xi) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iangalie uwezekano wa kuupatia Mkoa Boti imara na iwe ya kisasa kwa ajili ya kufanyia doria Baharini ili iwe rahisi kuratibu shughuli za doria ya kudhibiti uvuvi haramu katika pwani ya Halmashauri zote za Kilwa, Lindi na Manispaa ya Lindi.

xii) Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iangalie uwezekano wa kuanzisha kituo cha kuzalisha mbegu bora ya samaki (fingerlings) aina ya mwatiko (Milkfish) katika maeneo ya pwani kandokando mwa Bahari ya pwani ya Mkoa wa Lindi na ikiangalie kituo cha uzalishaji wa mbegu cha mtama kwa kukifanyia ukarabati ili kiweze kufanya kazi, sambamba na Halmashauri zione uwezekano wa kuanzisha mashamba darasa (mabwawa ya mfano) katika maeneo yao ili kuhamasisha wananchi suala la ufugaji samaki kupitia mabwwa hayo.